



**Muda:**

5 years  
(Jan. 2019 – Dec. 2023)

**Maeneo makuu  
lengwa:**

Site I: Halmashauri 12 kwenye mkoa ya Arusha, Kilimanjaro, na Tanga

**Wanufaika:**

~Makadilio. Kaya 4,000

**Watekelezaji:**

Wizara ya Kilimo na TAMISEMI\*  
Watendaji Kazi ni Kikosi kazi cha DADP\*\*

**Dhumuni:**

Kufanya DADPs zifanye kazi ili kufanikisha mapato makubwa kwa wakulima wa mbogamboga kupitia mbinu za SHEP.

**Mawasiliano:**

JICA TANSHEP  
Killimanjaro , Ofisi ya Mkuu wa Mkoa  
Moshi, Kilimanjaro  
Ms. Stella Andrea  
0752-224-763, Barua pepe

\* Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

\*\*Inausisha Idara ya sera na Mipango (DPP), Idara ya Uratibu wa Sekta (DSC), Idara ya Maendeleo ya Mazao (DCD), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Horti. Tengeru, na Tanzania Horticulture Association (TAHA)

SHEP huanza na "Utafiti wa Soko" hufanywa na wakulima. Baada ya kugundua mahitaji ya soko, wakulima watakuwa wako kimkakati kupanga mpango wao wa uzalishaji ili kuongeza faida. Hii ni pamoja na kuchagua mazao / aina, ubora wa mazao / muda wa kuvuna nk.


## Mradi wa Kuimarisha Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na Uwezo wa Utekelezaji kwa kutumia mbinu ya SHEP (TANSHEP)



(Picha: Kikundi cha Wakulima Lushoto, Tanga kikifanya Utafiti wa soko)

Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo (DPs) wamekuwa wakitekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) tangu mwaka 2003/04. Katika ASDP, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA) inaunda na kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP), kuendana eneo.

Mradi unakusudia kuimarisha uwezo wa Halmashauri kwa kuunda na kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP) kwa kuanzisha mbinu ya SHEP. Hivi sasa, wakulima wengi wa mazao ya mbogamboga wanalima bila kujua mahitaji ya soko. Mara nyingi husababisha kuuza mazao kwa bei ya chini au hata mazao mengi Kutouzika. Kupitia SHEP, vikundi vya wakulima vitabadilishwa kufuata "Kilimo kinacholenga Soko" na kuonyeshwa fursa nyingi (k.m. kutambulishwa kwa wanunuzi, wasambazaji, taasisi za kifedha n.k. tofautitofauti) kwa kuboresha mpango wa uzalishaji ili kupata faida kubwa.



# «Anzia Sokoni Malizia Shambani Kwa Kipato Zaidi»

	Hatua	Shughuli
0	Utafiti wa Awali Kumbukumbu za mapata ya Shambani	Wawezeshaji wa Wilaya (DFT) kwa kila Halmashauri wanawafundisha Vikundi vya wakulima & Maafisa Ugani kufanya utafiti wa awali
1	Utafiti wa Soko (Inajumuisha: Kuchagua Mazao)	Wawezeshaji wa Wilaya wanawasaidia vikundi vya wakulima kuandaa mpango wa utafiti wa soko, Vikundi vya Wakulima & Maafisa Ugani watafanya utafiti wa Soko, Vikundi vya wakulima watachagua zao la kuzalisha.
2	Kuunganishwa na Wadau (Mtandao)	Vikundi vya wakulima wataandaa maenezo marupi ili kujitangaza wenyewe, watakutana na wadau (k.m kampuni za usambazaji, mabenki n.k.) kujadili njia za kushirikiana.
3	Mpango Kazi	Vikundi vya Wakulima watafanya uchambuzi wa faida (uchambuzi wa gharama / faida), wataengeneza mpango wa uzalishaji (kalenda ya mazao) pamoja na programu za mafunzo,
4	Mafunzo shambani	Vikundi vya Wakulima vitabainisha mahitaji ya kiufundi juu ya kilimo ambacho maafisa ugani na wawezeshaji wa wilaya huandaa kwa ajili ya mafunzo shambani
5	Tathmini Kumbukumbu za mapato	Vikundi vya wakulima wataengeneza upya rekodi ya mapato ya shambani, kufanya tathmini ya uzalishaji wa majaribio ili kuendana na msimu ujao

## Hafla ya Kuunganishwa na Wadau



Kikundi cha wakulima

Wanunuzi

SHEP Handbook for Extension Staff (Picha : Ethiopia)


✓ Hafla ya kuunganishwa na Wadau (Inaweza kuwa Oct hadi Nov) inalenga

1. Kuonyesha fulsa za biashara
2. Kuanzisha uhusiano wa Kibiashara

✓ Stakeholders includes,:

- ❖ Wasambazaji wa pembejeo za kilimo
- ❖ Wanunuzi

### Ratiba



Mradi unatekelezwa kupitia ushirikiano wa ufundi kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA)